

# Magozwe

Ursula Nafula

Wiehan de Jager

Kiswahili





Kulikuwa na wavulana wa kurandaranda mtaani.

Mdogo wao alitwa Magozwe.



Wazazi wa Magozwe walikufa akiwa mdogo.

Alienda kuishi na mjombake.



Mjombake alimtesa.

Magozwe alitorokea mtaani.




Maisha ya mtaa yalikuwa magumu.

Waliishi kwa kuombaomba.



Siku moja, Magozwe aliokota kitabu cha hadithi kwenye  
pipa.



Picha zilionyesha rubani.

Magozwe alitamani kuwa rubani mashuhuri.



Magozwe alikuwa akiomba chakula barabarani.

Alikutana na Tomaso.





Tomaso aliwapeleka pahali walikopata chakula.



Siku moja, Magozwe alimwambia Tomaso, "Sijui kusoma."



Magozwe pia alimweleza kwa nini alitoroka kwa mjombake.



Magozwe alisherehekea miaka kumi ya kuzaliwa.

Tomaso alimpatia kitabu.



Magozwe alifikiria juu ya kwenda shule.



Ingawa aliogopa, Tomaso alimtia moyo.



Magozwe alipelekwa katika makao ya watoto.



Alisoma kwa bidii.





Siku moja, Magozwe alimweleza Tomaso, "Nitakuwa rubani maarufu kwa wote."

You are free to download, copy, translate or adapt this story  
and use the illustrations as long as you attribute in the  
following way: Lesley Koyi Author - Lesley Koyi

Adaptation - Ursula Nafula

Illustration - Wiehan de Jager

Language - Kiswahili

Level - First words © African Storybook Initiative 2015

Creative Commons: Attribution 4.0

Source [www.africanstorybook.org](http://www.africanstorybook.org)

